TANGAZO LA SERIKALI Na 209 la Tarehe15/8/2019

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 6(1) na 16(1)*

SHERIA NDOGO ZA(USHURU WA MAZAO YA UVUVI) ZA ALMASHAURI YA JIJI LA TANGA ZA MWAKA, 2019

## SEHEMU YA KWANZA
UTANGULIZI

Jina la sheria na muda wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Uvuvi)za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka, 2019, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokua pale itakapoelezwa vinginevyo:-

"Ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa umma aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi. "Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Tanga;

"BMU" maana yake ni Beach Management Unit (kikundi cha usimamizi wa rasilimali za uvuvi kwenye mialo

"Chombo cha usafiri majini" maana yake mtumbwi wa injini au kasi, jahazi, mashua, boti, ngarawa, dau au chombo chochote kitakachotumika kwa shughuli za uvuvi.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Tanga.

"Kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"Mwalo" maana yake ni eneo maalum kando kando ya mto, bahari au bwawa ambayo imewekwa kwa ajili ya kuegesha vyombo vya uvuvi.

"Mazao ya uvuvi" maana yake ni samaki, dagaa, konokono, mabondo, mwani, uduvi, au malighafi yoyote inayotokana na shughuli za uvuvi.

"Zana za uvuvi" maana yake ni vifaa vyote halali vinavyotumika kwa ajili ya shughuli za uvuvi ikiwemo nyavu, ndoano au madema.

"Zana haramu za uvuvi" ni vifaa vyote ambavyo kwa mujibu wa Sheria ,haviruhusiwi kutumika katika shughuli za uvuvi.

## SEHEMU YA PILI
### UTOZAJI WA USHURU

Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza kwa mtu yeyote Ushuru wa mazao yatokanayo na shughuli za uvuvi zinazofanyika ndani ya eneo la Halmashauri.

(2)Ushuru wa mazao ya uvuvi utatozwa na Halmashauri katika maeneo yote ya Mialo, masoko au maeneo mengine maalum yaliyotengwa kwa ajili ya kuuzia mazao yatokanayo na shughuli za uvuvi kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza laSheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kulipa Ushuru

5. Itakuwa ni wajibu kwa kila muuzaji wa mazao ya uvuvi kuhakikisha analipa ushuru kwa viwango vilivyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa Halmashauri.

6. Halmashauri itakuwa na wajibu wa;

a) kushirikiana na BMU (Kamati ya hifadhi) katika kusimamia shughuli za uvuvi katika eneo la Halmashauri;
b) kudhibiti biashara holela ya mazao ya uvuvi;
c) kudhibiti uvuvi haramu;
d) kushirikiana na vyombo vingine vya dola na kutumia ulinzi shirikishi kuimarisha ulinzi wa rasilimali na usalama wa

wavuvi.

e) kuunda Kamati Ndogo za ulinzi wa shughuli za uvuvi na Kamati ya Mazingira kattika mialo na maeneo yote yanayotumika kwa shughuli za uvuvi.

Kazi za Kamati

7. Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi Kamati Ndogo ya ulinzi kwa kushirikiana na Kamati ya Mazingira itakuwa na jukumu la kutenga maeneo kwa ajili ya kutoa huduma ya shughuli za uvuvi.

Leseni za uvuvi

8.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mvuvi kuwa na leseni ya uvuvi kutoka katika mamlaka husika, isipokuwa kwa wavuvi waendao kwa miguu (foot fishers).

(2) Mvuvi yeyote kutoka nje ya eneo la Halmashauri atakayetaka kufanya shughuli za uvuvi katika eneo la Halmashauri atalazimika kujisajili katika BMU/Kamati ya hifadhi.

Usajili wa wavuvi

9. Kila mvuvi atapaswa kusajiliwa katika kitabu cha wavuvi wote katika BMU/Kamati ya hifadhi akionyesha mmiliki wa chombo na namba ya usajili wa chombo hicho.

Maegesho ya vyombo vya uvuvi

10. Vyombo vyote vya kukusanyia samaki au kusafirisha mizigo au abiria itaegeshwa umbali wa mita 10 (kumi) kutoka kwenye uzio.

Uhakiki wa ubora wa mazao ya uvuvi

11.-(1) Magari yote yatakayobeba samaki yatakuwa magari maalum yenye cheti kutoka kwa Afisa Mfawidhi wa udhibiti wa ubora wa samaki na viwango.

(2) Magari yote maalum yatapaswa kuwa na nembo ya samaki ubavuni na picha ya samaki.

(3) Magari hayo yasiwe na vumbi au kutu.

(4) Magari yawe na milango iliyotengenezwa kwa kutumia vifaa vinavyokubalika katika viwango vya ubora

Makosa

12.-(1) Mtu ye yote atakuwa ametenda kosa endapo :-

(a) ataingizakilevi cha aina yoyote, kunywea kilevi cha aina yoyote ndani ya uzio wa mwalo au Soko la samaki.

(b) atauzia mazao ya uvuvi nje ya maeneo yaliyotengwa maalumu kwa ajili ya kuuzia mazao hayo.

(c) ataweka samaki chini au juu ya paa la tishari, darajani au juu ya gari aukwenye mchanga.

(d) atashawishi wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi kugoma kulipa ushuru wa mazao ya uvuvi .

(e) kutorosha mazao ya uvuvi bila ya kuyalipia ushuru

(f) kufanya shughuli za uvuvi na biashara ya kuuza mazao ya uvuvi bila ya kuwa na leseni halali.

(g) kutumia zana haramu za uvuvi.

(h) kutupa taka au kuchafua mazingira katika eneo lote la mwalo/Soko.

(i) kuoga, kufua nguo, kuosha vyombo na kunawa kwa kutumia sabuni katika eneo la maji ya mwalo umbali wa mita 200 kulia au kushoto kwa tishari au Uzio.

(j) kubeba samaki katika gari maalum ya kubebea samaki ikiwa na barafu chafu kwa ajili ya kuhifadhia samaki ili wasiharibike.

(k) kuuza samaki walioharibika.

(l) Kutumia chombo cha uvuvi kisichokuwa na namba ya usajili na inayoonekana kwa ufasaha.

(m) kupima mazao ya uvuvi kwa kutumia mzani ambayo haina nembo ya wakala wa vipimo.

(n) kutumbua samaki mwaloni na kutupa utumbo na mabaki ya samaki hovyo kwenye eneo majini au nchi kavu.

Adhabu

13. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa, na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni Moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

14. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza faini isiyopungua shilling laki mbili (200,000/=) au isiyozidi Shillingi laki tano (500,000/=) mtu yeyote endapo Mkosaji kwa hiari yake mwenyewe atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kulipa kiasi cha ushuru anachodaiwa na faini kwa kujaza fomu maalum kama ilivyoonyeshwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

*Tangazo la Serikali Na. 209 (linaendelea)*

JEDWALI LA KWANZA
*(Kifungu cha 4(2)*

USHURU WA MAZAO YA UVUVI

| NA | AINA YA USHURU | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Minada ya samaki katika mwalo au eneo maalum la kuuzia | Asilimia Tano (5%) ya bei ya mazao |
| 2. | Ushuru wa mazao ya uvuvi bila ya kutumia mnada | |
| | i. Gunia la dagaawakavu kwa vipimo vifuatavyo: | |
| | (a) Chini ya kilo 50 | Tsh.5,000 kwa gunia |
| | (b) Kuanzia kilo 51 hadi kilo 100 | Tshs. 10,000 kwa gunia |
| | (c) Kuanzia kilo 101 | Tshs.15,000 kwa gunia |
| | ii) Samaki wabichi | Tshs. 100/= kwa kilo |
| | iii) Gunia la konokono la uzito wa kilo 100 | Tshs.1,500/= |
| | iv) Ushuru wa kuegesha (kutia nanga) kwa vyombo vya kigeni | Tshs.2,000/= kwa siku |
| | v) Ushuru wa mazao yanayoletwa na vyombo kutoka nje:- | |
| | (a) Mazao mengine ya uvuvi | Tsh. 300/= kwa kilo |
| | vi) Mawe na mapambo ya majini | |
| | (a) Kilo 1 hadi 500 | Tshs. 5,000/= |
| | (b) Kilo 501 hadi 1,000 | Tshs 20,000/= |
| | (c) Zaidi ya kilo 1,000 | Tshs 30,000/= |

JEDWALI LA PILI
HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA
*(Chini ya kifungu cha 14)*

Mimi ……………………………………wa S.L.P. …………, …………………………………. nakiri kutenda kosa la ……………………………………………………………….. ikiwa ni kinyume na kifungu cha ……………… cha Sheria Ndogo za (Ushuru wa Mazao ya Uvuvi) za Halmashauri ya Jiji la Tanga za Mwaka ,2019.
Kwa hiyo, kwa hiari yangu mwenyewe pasipo kushawishiwa na mtu yeyote nakubali kulipa faini iliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hizi iwapo Mkurugenzi atatekeleza madaraka aliyopewa chini ya kifungu cha 14 cha Sheria Ndogo hizi.

Saini: ………………………………………………...

Mbele yangu:-
Jina: ………………………………………………..…..
Saini: ………………………………………………..…..
Wadhifa: ………………………………………………...

Lakiri ya Halmashauri ya Jiji la Tanga imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Tanga kilichofanyika Tarehe 30 mwezi Januari mwaka 2019 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikibandikwa mbele ya:-

L.S

……………………………………………………

DAUDI R. MAYEJI,
*Mkurugenzi wa Jiji*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

……………………………………………………

SELEBOSS M. MUSTAFA,
*Mstahiki Meya*
*Halmashauri ya Jiji la Tanga*

NAKUBALI,

Dodoma,
1 Machi, 2019

SELEMANI S. JAFO (MB.),
*Waziri wa Nchi ofisi ya Rais TAMISEMI*